

Je, dhamana ni nini?

Produced by the Paralegal Advisory Service (PAS) 2004



1 Je, dhamana ni nini ?

Dhamana ni kitendo cha mshukiwa kuachiliwe huru kwa muda, huku akingojea kusikizwa kwa kesi baada ya kulipa pesa kiasi fulani.



4 Je, dhamana hukubaliwa aghalabu?

Ndio, dhamana inapaswa kukubaliwa aghalabu isipokuwa kama kosa ni zito sana na kuna hatari kwamba mshukiwa atatoroka au kuwatisha mashahidi, au kutenda makosa mengineyo au kusumbua utulivu wa umma, na hapo wanaondesha mashtaka huweza kupinga ombi la dhamana.



5 Je, utafanya nini endapo utakatazwa dhamana?

Unaweza kukabiliana na upingamizi kwa kuhakikisha mahakama kwamba:

- o Una makao yakudumu na kuonyesha kuwa una uhusiano wenye nguvu katika jamii (kwa kumwita kasis au mwalimu au mtu mwingine yeyote katika jamii anayeheshimika)
- o Unaweza kumleta mtu atakayelipa mahakama kiasi fulani cha pesa kama hakikisho kuwa utafika mahakamani siku ya mashtaka (mdhamini).

2 Ni nani hukubali kutolewa kwa dhamana?

Mahakama, pamoja na /au maafisa wakuu wa polisi.

3 Je, ninapaswa kupata dhamana wakati gani?

Punde tu baada ya kukamatwa na kufukishwa katika kituo cha polisi ama wakati wako wa kwanza kufukishwa mahakamani.

6 Kwa hiyo ni bora washukiwa wengi wanapaswa kukubaliwa dhamana?

Ndiyo, katiba yasema wazi " Kila mtu aliyekamatwa au kushtakiwa kwa kosa atakuwa na haki ya kuachiliwa kutoka kizuizini akiwa au asipokuwa na dhamana mradi tu sio kinyume na utendaji wa haki.




7 Ni nani anayeamua kama "manufaa ya haki" yamezingatiwa kabla ya dhamana?

Ni mahakama

8 Je, dhamana ikikataliwa mambo huishia hapo?

La, unaweza kuiomba tena mahakama kama mambo yamebadilika tangu uliponyimwa mwanzoni – kwa mfano, jamaa yako akikupatia mahali pa kukaa au alete kiasi fulani cha pesa kama dhamana. Unaweza pia kukata rufaa katika mahakama nyingine ya kiwango cha juu.



9 Je, dhamana ikikubaliwa hutokea nini?

Unakubaliwa kwenda nyumbani na kuendelea na maisha yako ya kawaida hadi utakapo hitajika kurudi mahakamani ili kesi yako itajwe au isikilizwe.

